# GRADE 4 MID TERM 2 MAY 2022

## KISWAHILI

# TARGETER WINGS

## KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

## GREDI 4 - 2022

Wings 002

## KISWAHILI : INSHA

Jina: ..............................................................................................

Jina la shule: ..............................................................................................

| Viwango vya kutathmini | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kuzidisha matarajio | Kufikia matarajio | Kukaribia matarajio | Mbali na matarajio |
| Kuandika | 9 - 10 | 6 - 8 | 3 - 5 | 0 - 2 |

*Kuandika (Alama 10)*

***Andika insha ya kusisimua kuhusu:***

**SHEREHE NYUMBANI KWETU**

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

# TARGETER WINGS

## KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

## GREDI 4 - 2022

Wings 002

# SHUGHULI ZA KISWAHILI

Jina ..........................................................................................................................

Jina la shule ..............................................................................................................

**Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi.**

| Viwango vya kutathmini | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kuzidisha matarajio | Kufikia matarajio | Kukaribia matarajio | Mbali na matarajio |
| Kusikiliza na Kuzungumza | 5 | 4 | 3 | 0 - 2 |
| Kusoma kwa sauti | Maneno 71 na zaidi | Maneno 51-70 | Maneno 25 - 50 | Maneno 0 - 24 |
| Sarufi | 19 - 20 | 13 - 18 | 6 - 12 | 0 - 5 |
| Ufahamu | 10 | 7 - 9 | 4 - 6 | 0 - 3 |

## I. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA (alama 5)

***Sikiliza mwalimu kisha ujibu maswali***

a) Kitanda hupatikana katika sehemu gani ya nyumba? ***(Mwanafunzi ajibu)***

b) Mtu akikuamkua sabalkheri utajibu vipi? ***(Mwanafunzi ajibu)***

c) Je, siku njema ni maagano yanayotumika wakati gani? ***(Mwanafunzi ajibu)***

d) Mkiwa na marafiki wako mkicheza, mmoja wenu aumie, je mtafanya nini kwanza kabla ya kwenda hospitalini? ***(Mwanafunzi ajibu)***

e) Kifaa kinachotumika kufagia darasani kinaitwaje? ***(Mwanafunzi ajibu)***

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

## II. KUSOMA KWA SAUTI.

***Soma kifungu hiki kwa sauti mwalimu akisikiliza.*** **(Alama 10)**

Hospitali ni mahali ambapo maradhi hutibiwa. Wagonjwa hujipeleka wenyewe hospitalini na wale mahututi hupelekwa kwa ambulensi. Mtu akiwa mgonjwa sana hubebwa kwa machela kutoka kwenye ambulensi.

Ili kujua matatizo ya mgonjwa, muuguzi au daktari humpima kwanza. Kifaa kinachotumiwa kumpima mgonjwa sanasana ni kipimajoto. Mgonjwa akiumwa na tumbo, itabidi choo chake kichunguzwe na darubini maalum ya daktari. Akiwa ana kifua kikuu, basi atapigwa picha ya eksirei. Hii ni picha maalum inayoonyesha sehemu za mwili za ndani. Mgonjwa wa kifuakikuu huwa anakohoa sana.

## III. KUSOMA UFAHAMU

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.** **(Alama 5)**

Ilikuwa ni sikukuu ya mji. Watu wa kaunti ya Duro walikuwa wakisherehekea siku ya kuanzishwa kwa kaunti hiyo. Wananchi wote wa wilaya hiyo walihudumiwa. Kulifanywa karamu kubwa.

Watoto wa shule zote za wilaya hiyo walihudhuria na waliimba nyimbo tamutamu. Pia kulikuwa na ngoma za kienyeji. Siku hiyo ilikuwa ya furaha tele. Watu walikuwa wakicheza huku wameshikilia wanyama. Walikuja na mbuzi na kondoo. Viongozi wote waliwahutubia wananchi. Kila aliyesimama aliwahimiza wananchi wawe na amani.

Watoto wa shule waliimba nyimbo nzuri sana. Hata mgeni wa heshima alisimama na kucheza pamoja na watoto hao. Watoto nao walipewa zawadi nyingi. Wageni wote waliohudhuria walipewa zawadi. Baadaye karamu ilianza. Watu walikula na kunywa kwa furaha. Mwishowe watu waliondoka huku wakiimba nyimbo za kupendeza.

**Maswali**

1. Watu wa kaunti ya Duro walikuwa wakisherehekea nini? (Alama 1)

______________________________________________

2. Ni akina nani walihutubia wananchi wa kaunti ya Duro? (Alama 1)

_______________________________________________

3. Viongozi waliwahimiza wananchi kuzingatia nini? (Alama 1)

_______________________________________________

4. Neno jingine la 'sherehe' ni ____________________ (Alama 1)

5. Watu walifanya nini wakati walipokuwa wakiondoka? (Alama 1)

_______________________________________________

**Soma ufahamu huu kisha ujibu maswali yafuatayo**

Kulikuwa na mvuvi mmoja aliyeitwa Kairo. Alikuwa maskini. Hali yake ilikuwa duni sana. Alikuwa hana lolote hana chochote. Hata hivyo alijikaza kisabuni, hakukata tamaa kama wavuvi wengine.

Kila siku alifanya bidii ili kuinua hali yake ya maisha. Alielewa kuwa haba na haba hujaza kibaba. Alifanya bidii za mchwa ili apate lishe bora kwa wanawe watatu na mkewe. Alifanya bidii kwani alielewa kuwa mgaagaa na upwa hali wali mkavu. Aliweza kununua dau kubwa ajabu. Mle ndani aliweka majokofu angalau kuhifadhi samaki. Alijua akiba haiozi.

Kairo hakukoma kufanya bidii. Aliamka saa kumi na mbili na kuelekea baharini. Katika pilkapilka hizo alibeba sime iliyotiwa makali, ingawa hakujua sababu ya kuibeba. Alfajiri moja kama ilivyokuwa kawaida yake aliondoka kabla ya jua kuchomoza. Alienda hadi ufuoni mwa ziwa. Alitupa nyavu zake majini huku akiwa na matumaini kwamba Mungu angemjalia. Hata hivyo juhudi sio pato. Alienda mbali zaidi na ikawa hangeweza kuendelea sana kutokana na uzito wa nyavu. Alijua kwamba angesahau shida kama alivyosahau kunyonya. Alirudi hadi ufuoni na kuvuta nyavu zake. Mwanzoni aliwaona samaki wakubwa wakubwa. Alivyozidi kuvuta kumbe mle ndani mlikuwa na mamba wawili wakubwa ajabu.

**Maswali**

6. Mvuvi ni nani? (Alama 1)

_______________________________________________

7. Kairo alifanya bidii akaweza kununua nini? (Alama 1)

_______________________________________________

8. Kairo aliweka nini ndani ya dau ili kuhifadhi samaki? **(Alama 1)**

_______________

9. Kairo aliamka saa ngapi kuelekea baharini? **(Alama 1)**

_______________

10. Ni nini ilifanya nyavu zake Kairo kuwa nzito? **(Alama 1)**

_______________

**SARUFI.** **(Alama 20)**

**A. Tumia sisi, wewe, yeye au wao badala ya maneno yaliyopigiwa mstari.** **(alama 4)**

1. Kamau na Ochieng' wanapenda kucheza kadanda. _______________
2. Daudi anapenda kuchora. _______________
3. Mimi na mama yangu tutasafiri kwenda Mombasa. _______________
4. Masengo utakula chakula gani? _______________

**B. *Ambatanisha maamkuzi haya na majibu yake.*** **(Alama 3)**

| | **Maamkuzi** | **Majibu** |
|---|---|---|
| 5. | U mzima? | Njema |
| 6. | Hamjambo? | Ni mzima |
| 7. | Uhali gani? | Hatujambo |

**C. Tunga sentensi ukitumia maneno haya.** (Alama 4)

8. Kifupi _______________
9. Cheka _______________
10. Chumba _______________
11. Mgeni _______________

**D. Tegua vitendawili vifuatavyo.** **(Alama 2)**

12. Jicho la Mungu linachoma. _______________
13. Huku ng'o na kule ng'o _______________

**E. Andika sentensi hizi kwa wingi.** (Alama 4)

14. Mtoto ameenda kununua kitabu. _______________
15. Mti huu ulipandwa na mwalimu. _______________
16. Kitabu hiki ni changu. _______________
17. Nguo hii ni ya mgeni. _______________

**F. Kanusha sentensi zifuatazo** (Alama 3)

18. Anaenda shuleni _______________
19. Alifika asubuhi sana _______________
20. Mama anapika kuku _______________